Aflasafe™ hutumika katika kiwango cha kilogramu 4 kwa ekari moja(kilogram 10 kwa hekta moja) ambacho hutawanywa shambani majuma mawili hadi matatu kabla ya mahindi kutoa mbelewele na siku 30-45 baada ya kupanda karanga.

Wakulima wakitawanya Aflasafe™

Mlo kamili ulio na vyakula mbalimbali

Dkt. Maria Musa anawaeleza kwa ufupi wanakijiji jinsi ya kupunguza uwezekano wa kupata sumukuvu kwa kula mlo bora wenye aina tofauti za vyakula.

Ili kupunguza viwango vya sumukuvu kwenye vyakula vyetu inatupasa kula milo tofauti; inabidi kuhakikisha tunakula aina mbalimbali za vyakula. Hii haipunguzi tu uwezekano wa kula vyakula vyenye uwezekano mkubwa wa kupata sumukuvu bali pia inaboresha afya.

Baadhi ya vyakula kwa mfano, vile vinavyotokana na mahindi na karanga vina uwezekano mkubwa wa kupata sumukuvu. Vyakula kama viazi mviringo/ vitamu, wali na mboga za majani havihathiriwi na sumukuvu. Hivyo, inashauriwa kula kiwango kidogo cha vyakula vitokanavyo na mahindi kama vile ugali. Nivyema kuongeza kiasi kidogo cha viazi mviringo/ vitamu, wali, magimbi, mboga za majani n.k.

Pia, hakikisha unakula kiasi cha protini kama vile, nyama, kunde, matunda na mboga za majini kila siku.



Pia hakikisha unakula vyakula vya aina zote. Vyakula vyenye wanga, protini, matunda na mboga za majani n.k.

Kipeperushi hiki kimeandaliwa na kuchapishwa kwa msaada wa Watu wa Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID). IITA inawajibika kwa yaliyomo kwenye kipeperushi hiki na wala sio msimamo au maoni ya USAID au Serikali ya Marekani.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
George Mahuku
Taasi ya Kilimo cha Kitropiki,
Ukanda wa Mashariki IITA -Tanzania
S.L.P Box 34441
Dar es Salaam - Tanzania
Simu +255 22 2700092
Fax:+255 22 2775021
Barua pepe: g.mahuku@cgiar.org

Beatrice Pallangyo
Idara ya Afya ya Mimea
Wizara ya Kilimo
S.L.P. 2182
Dodoma - Tanzania
Simu: +255 26 2321407
Barua pepe: beatricepallangyo@yahoo.com

Ijue Sumukuvu

Maana, athari na udhibiti wake

Kufuatia vifo vya watu watano (watu wazima wawili na watoto watatu) vilivyotokea Wilaya ya Masikitiko kutokana na athari za sumukuvu, kikundi cha wataalam wanatembelea kijiji hadi kijiji kuelemisha umma/jamii kuhusu sumukuvu. Leo wataalam hao, Dkt.Joseph Mlinge kutoka Wizara ya Kilimo na Dkt.Maria Musa kutoka Wizara ya Afya, wamewasili katika kijiji cha Mambo Mema. Watawaelezea wanakijiji kuhusu sumukuvu, jinsi inavyosambaa, athari zake na jinsi ya kuidhibiti.

Sumukuvu ni nini?

Sumukuvu ni aina ya sumu inayozalishwa na fangasi au kuvu ambao hukaa kwenye udongo na masalia yaliyooza shambani. Hivyo, mazao mengi huathirika na sumukuvu yakiwa shambani.





Mazao ambayo hushambuliwa zaidi na kuvu hawa ni mahindi na karanga.

Sumukuvu pia hupatikana kwenye maziwa ya mama mzazi aliyekula chakula chenye sumukuvu na pia huweza kumuathiri mtoto kipindi cha kunyonyesha.



Vilevile sumukuvu hupatikana kwenye bidhaa za mifugo kama vile maziwa, mayai, na nyama, endapo mifugo itakuwa imelishwa vyakula vyenye sumukuvu.

Je nini viashiria vya Sumukuvu?



Fangasi wanaozalisha sumukuvu wana rangi ya kijani manjano. Nafaka yenye rangi ya kijani manjano inaweza **ikawa au isiwe** na sumukuvu. Mahindi au karanga yanaweza yasiwe na dalili za fangasi hawa lakini yakawa na kiasi kikubwa cha sumukuvu.



Athari za Sumukuvu ni zipi?

Dkt. Maria Musa anawaeleza kwa ufupi wanakijiji kuhusu athari za sumukuvu kwa wanadamu, wanyama, biashara na masoko.

1. Binadamu
Watu wanapokula chakula chenye sumukuvu kwa miaka mingi wanaweza kupata saratani ya ini na kinga ya mwili hudhohofika.



Saratani ya Ini

Upungufu wa kinga mwilini

Watoto hudhoofika mwili na dalili zake ni uzito mdogo, utapia mlo na kudumaa.

Utapiamlo

Mtoto aliyedumaa

Vifo! Chakula chenye kiwango kikubwa cha sumukuvu huweza kusababisha vifo.



2. Mifugo!
Sumukuvu huathiri mifugo. Kwa mfano, kwa mifugo jamii ya Kuku, sumukuvu hudumaza ukuaji na uzalisha wa mayai.



Kuku aliye athirika na malisho yenye sumukuvu

3. Biashara na Masoko
Sumukuvu huathiri soko. Mazao yaliyoathirika na sumukuvu hukosa soko la ndani na nje ya nchi. Hii inasababisha ukosefu wa mapato.

Tunawezaje kudhibiti Sumukuvu?

Wanakijiji wamekwisha jifunza kuhusu sumukuvu na athari zake. Swali lilliofuata ni njia za kudhibiti sumukuvu.

Mbinu bora za kilimo

Kanuni hizi ni pamoja na;

a) *Kuvuna:* Vuna mazao baada ya kukauka vizuri na hakikisha gunzi haligusani na udongo

b) *Kuchambua:* Tenganisha magunzi yenye mahindi ambayo hayajakauka vizuri au yaliyoharibiwa na visumbufu kabla ya kukausha na kuhifadhi.

c) *Kukausha:* Sambaza mahindi kwenye sehemu iliyoinuka, weka juu ya kifaa cha kuanikia kwa mfano; turubai ili kuzuia yasigusane na udongo.

d) *Kuhifadhi:* Hifadhi mazao kwenye sehemu kavu na isiyo na joto. Weka mifuko yenye nafaka sehemu iliyoinuka kwa mfano juu ya mbao. Dhibiti visumbufu ghalani, kama vile dumuzi, wakati wa kuhifadhi. Hakikisha nafaka hazinyeshewi.



Namna nzuri ya kuanika juu ya turubali

Kuchambua kabla ya kuhifadhi

Uhifadhi unaofaa

Matumizi ya AflasafeTZ

Tunaweza pia kutumia mbinu salama na ya gharama nafuu ya kibaiolojia kwa kutumia AflasafeTZ. AflasafeTZ imetengenezwa na kuvu wasiozalisha sumukuvu. Kuvu hawa wanapotawanywa shambani huwaondoa kuvu wale wanao zalisha sumu.

Aflasafe™ imetengenezwa na Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA) kwa kushirikiana na Kitengo cha Utafiti idara ya Kilimo Marekani (USDA) na washirika wengine. Aflasafe™ ni salama na ina uwezo wa kudhibiti sumukuvu kwenye mazao kwa kiwango cha hadi asilimia 99. IITA imeshirikiana na Wizara ya Kilimo (WK) kutengeneza bidhaa mahususi kwa Tanzania, AflasafeTZ iliyosajiliwa hapa nchini mwaka 2018.